PHILADELPHIA GAS WORKS
800 W. MONTGOMERY AVENUE
PHILADELPHIA, PA 19122-0050

# TAARIFA YA KUFUNGWA KWA MITA KWA SIKU 3
## Huenda Huduma Yako ya Gesi Ikafungwa!

**Tarehe: ________________________________**

**Jina la Mteja: _____________________** **Namba ya Akaunti ya Mteja: _______________________**

**Anwani ya Huduma: ___________________________________________________________________**

**Huduma ya gesi ya anwani iliyo hapo juu itafungwa kufikia au baada ya saa 8:00AM tarehe _________________ kwa sababu hujaruhusu PGW kufikia mita yako. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu taarifa hii, tafadhali piga simu kwenye ofisi yetu kwa 215-235-1000.**

**<u>Hatutafunga huduma ya gesi ukifanya yafuatayo:</u>**

- Ukiruhusu tufikie mita yako kabla ya tarehe ya kufungwa iliyopangwa
- Ukipiga simu ili kupanga miadi kwa (215) 235-1000

**<u>Tukifunga huduma yako ya gesi, huenda ukalazimika kulipa ada ya ulinzi, ada ya kurudishiwa na ada ya kuchimba.</u>**

**TAARIFA YA DHARURA YA KIMATIBABU**

TUFAHAMISHE IKIWA KUNA MTU ANAYEISHI NYUMBANI KWAKO AMBAYE NI MGONJWA SANA AU ANA UGONJWA UTAKAOZIDI KUTOKANA NA KUFUNGWA KWA HUDUMA HIYO. HATUTAFUNGA HUDUMA YAKO wakati wa ugonjwa huo mradi:

1. Daktari wako mwenye LESENI, msaidizi wa daktari au muuguzi anayetibu wagonjwa atathibitisha kwa maandishi kuwa ugonjwa huo upo na kuwa unaweza kuzidi ikiwa huduma yako itasimamishwa; na
2. Utaweka mpango wa kulipa bili zako za sasa.
3. Utawasiliana nasi kwa kupiga simu kwa 215-235-1000
4. DAKTARI WAKO MWENYE LESENI, MSAIDIZI WA DAKTARI AU MUUGUZI ANAYETIBU WAGONJWA ATATUMA BARUA KWA PGW NDANI YA SIKU 3 INAYOTHIBITISHA UGONJWA HUO.

Ikiwa wewe ni mwathiriwa wa dhuluma na una amri iliyotolewa na mahakama, unaweza kupata ulinzi na taratibu maalum za matibabu ya dharura. **Tupigie simu mara moja kwa 215-235-1000 utufahamishe ili uweze kupata ulinzi na taratibu hizi maalum**. Tutahitaji utupatie nakala ya amri ya mahakama.

**JAMBO MUHIMU LA KUJUA – KABLA HATUJAFUNGA HUDUMA YAKO YA GESI**

- Ikiwa una maswali au unahitaji maelezo zaidi, tafadhali tupigie simu leo kwa 215-235-1000. Baada ya kuzungumza nasi, ikiwa hujaridhika, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume ya Huduma za Umma (Public Utility Commission, PUC). PUC inaweza kuchelewesha kufungwa kwa huduma ukiwasilisha malalamiko kabla ya tarehe ya kufungwa. Ili uwasiliane nao, piga simu kwa (800) 692-7380 au utume barua kwa: Pennsylvania Public Utility Commission, Box 3265, Harrisburg, PA 17105-3265.
- Ikiwa una amri halali ya **Kulindwa Kutokana na Dhuluma** au amri iliyotolewa na mahakama inayotambulika katika Jimbo hili inayothibitisha wazi kuwa wewe ni mwathiriwa wa dhuluma za nyumbani, unaweza kupata ulinzi wa ziada. **Tupigie simu mara moja kwa 215-235-1000**. Tutahitaji utupatie nakala ya amri hiyo na bado tutahitaji uturuhusu tufikie mita yako.
- Tupigie simu ikiwa bili yako hulipwa na mwenye nyumba. Unaulinzi fulani wa kisheria.
- Ikiwa unatatizika kuelewa au kuzungumza Kiingereza, tupigie simu ili upate huduma ya ukalimani bila malipo.
- Tafadhali wasiliana nasi ikiwa wewe ni mlemavu na unahitaji usaidizi.

Huduma yako ikifungwa:

- Tutahitaji uturuhusu tufikie mita yako ili tukurejeshee huduma na unaweza kutakiwa kulipa bili zozote ambazo umechelewa kulipa ili tukurejeshee huduma hiyo.
- Watu wote wazima wanaoishi nyumbani, ambao majina yao yapo kwenye mkataba wa kukodisha au mkopo wa nyumba wanachukuliwa kuwa 'mteja' na wana jukumu la kulipa bili.
- Mtu YEYOTE mzima ambaye amekuwa akiishi nyumbani anaweza kulazimika kulipa bili yote au sehemu ya bili ili arejeshewe huduma.
- Tunaweza kuchukua hadi siku saba kukurejeshea huduma.